**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/EZ/2024/34**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2025-00000003**

**SALUMU IDDI MLECHE............................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MTWARA (MTUWASA) ......................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 28 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 28 mwezi Februari 2025 kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe mambo yafuatayo: -

(i) arejeshe huduma ya maji kwa Mlalamikaji;
(ii) afute ankara ya maji kiasi cha TZS 128,007.75; na
(iii) amlipe fidia kwa kipindi ambacho Mlalamikaji alisitishiwa huduma ya maji.

Mnamo tarehe 31 Disemba 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Salumu Iddi Mleche wa Mtaa wa Penisula Kata ya Ligula Mkoani Mtwara akiwakilishwa na Lisa Sabato pamoja na EWURA CCC (Mlalamikaji) dhidi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa

Mazingira Mtwara (MTUWASA) (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumsitishia huduma ya maji na kumpatia ankara isiyo halali kwani haiendani na matumizi yake.

Mlalamikaji anadai kuwa mnamo Septemba 2024 Mlalamikiwa alimtoza ankara ya kiasi cha TZS 128,007.75 ikiwa ni ankara ya matumizi kwa mwezi mmoja, ambapo anadai kwamba matumizi yake ya mwezi hayawezi kufikia ankara ya kiasi bishaniwa. Mlalamikaji anaeleza kwamba mwezi ambao Mlalamikiwa amemletea ankara hiyo kubwa isiyo halali yeye hakutumia huduma ya maji ndani ya mwezi huo, hivyo mara baada kupokea ankara aliwasiliana na ofisi ya Mlalamikiwa.

Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba aliandika barua ofisi ya Mlalamikiwa kulalamikia ankara bishaniwa ya kiasi cha TZS 128,007.75 lakini hakupata muafaka wa Malalamiko yake ndipo aliamua kuwasilisha Malalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA) kwa utatuzi.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 03 Januari 2025, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 28 Januari 2025, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kuwa Mlalamikaji ni mteja wake na anakiri kupokea Malalamiko yake, akaendelea kueleza kwamba Mlalamikaji alipatiwa ankara bishaniwa kutokana na ubovu wa dira na kupelekea kupata ankara kubwa. Alifafanua kuwadira hiyo mbovu imebadilishwa katika eneo la Mlalamikaji na ankara bishaniwa imeshafutwa.

Mnamo tarehe 06 Februari 2025, kikao cha usuluhishi baina ya pande mbili kilifanyika katika ukumbi wa mkutano wa Hoteli ya Lavila Nouville mkoani Mtwara. Katika kikao cha usuluhishi Mlalamikiwa alieleza kwamba Mlalamikaji alipata ankara ambayo ni kubwa kutokana na ubovu wa dira ya maji ambayo imefungwa katika eneo lake, hivyo walifanya mazungumzo na Mlalamikaji na tayari wamebadilisha dira pamoja na kumrejeshea huduma ya maji Mlalamikaji ili aweze kuendelea kupata

huduma hiyo, Mlalamikiwa alieleza pia kuwaamefuta deni la kiasi cha TZS 98,000 kuanzia tarehe 22 Januari 2025 katika akaunti ya Mlalamikaji kutoka kwenye kiasi bishaniwa na kiasi kilichobakia ni TZS 30,007.75. Mlamikiwa alitoa taarifa kuwa Mlalamikaji amelipa kiasi cha TZS 30,007.75 ikiwa ni matumizi ya mwezi Septemba 2024.

Kwa upande wa Mlalamikaji aliwakilishwa na EWURA CCC alisema kuwa kutokana na Mlalamikiwa kutekeleza hayo yote hana nia ya kuendeleza Malalamiko baina yao hiyo anaamua kuondoa Malalamiko yake. Mnamo tarehe 12 Februari 2025, Mlalamikaji aliwasilisha ujumbe mfupi wa maneno kwa njia ya simu wa kuondoa malalamiko yake kutokana na utekelezaji wa Malalamiko yake.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 28 mwezi wa Februari 2025.

.............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**